# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

## Mkataba wa Huduma kwa Mteja

# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

## Mkataba wa Huduma kwa Mteja

## YALIYOMO:

DIBAJI........................................................................................................ 1

LENGO LA MKATABA HUU............................................................................ 2

Mambo Muhimu katika mkataba wa huduma kwa wateja .................................................................. 2

Mapitio ya Mkataba ..................................................................2

MISINGI YA UTOAJI HUDUMA KWA UMA .......................................................3-4

WATEJA WETU ..........................................................................................4-5

VIWANGO VYETU.......................................................................................6-7

HUDUMA ZETU ...........................................................................................7

MALENGO YETU..........................................................................................7

MAADILI MUHIMU.........................................................................................8

VIWANGO VYETU.......................................................................................8-9

MALALAMIKO ..............................................................................................10

Haki na majukumu ya Wateja.......................................................10

UFUATILIAJI WA MALALAMIKO ...................................................10

Jinsi ya kutuma Malalamiko..........................................................11

Namna ya kutoa mrejesho wa Maendeleo ya Mkataba..............11

Kumbukumbu za Malalamiko ......................................................11

Kukata Rufaa .................................................................................12

MAPITIO YA MKATABA ...........................................................................12

UTOAJI WA TAARIFA.................................................................................13

Ushauri katika Mapitio ..............................................................................13

## MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA

### DIBAJI

Mikataba ya Huduma kwa Wateja ni "**makubaliano ya kijamii**" kati ya watoa huduma na wapokea huduma hizo. Mkataba huu unainisha viwango vya huduma ambavyo tunaamini wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza wanaitarajia katika ufuatiliaji na utatuzi wa matatizo pale yanapojitokeza. Mikataba huandaliwa kwa kuwashirikisha wateja pamoja na watumishi. Ni jambo zuri kwa Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuwa Halmashauri ni mojawapo iliyoanzisha mfumo huu na kuhakikisha kuwa inatoa ripoti za kila mwaka, kwa wadau kuhusu mafanikio ya mkataba huu. Mfumo wa ufuatiliaji na utathimini tuliouanzisha kwenye program ya uboreshaji wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza utatusaidia sana katika jambo hili.

Dhana na utekelezaji wa mikataba ya huduma imekuwa ikipata msukumo mkubwa kutoka Serikali Kuu. Halmashauri imetambua umuhimu wa kutumia mikataba ya huduma kama chombo cha kuleta mabadiliko Kiuchumi na Kiutamaduni kuelekea mfumo wa huduma ambao unamlenga zaidi mteja ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Ili uweze kufanya kazi vema inabidi mkataba huu uwe hati hai inayotokana na mahusiano mazuri ya kikazi tunayotarajia kuyajenga kati yetu, wateja na watumishi. Ninaupendekeza mkataba huu kwenu wote nikitarajia kuwa mtazitumia mbinu zilizopendekezwa ndani yake kuweza kuwa katika maelewano mazuri ya kikazi na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kufikia lengo letu la kuzipitia na kuziboresha huduma zetu kila mara.

Kiomoni Kiburwa Kibamba
**MKURUGENZI WA JIJI**
**MWANZA**

## LENGO LA MKATABA HUU

Lengo kuu la Mkataba wa huduma kwa wateja ni kukuza uelewa wa upatikanaji na ubora wa huduma zitolewazo na Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kuwasaidia wananchi kuelewa shughuli zetu, namna ya kutupata, viwango gani vya huduma wategemee kutoka kwetu na jinsi ya kutatua matatizo yanapojitokeza. Mkataba utawasaidia wahusika katika kudai haki zao, na pia unatoa uwazi zaidi katika kutupata na kutoa malalamiko kuhusiana na huduma zetu.

### Mambo Muhimu

Katika kufanikisha azma hii, mkataba huu unajumuisha mambo yafuatayo:-

1. Kuelewa kwa undani kuhusu wateja wetu na huduma ambazo ni muhimu kwao.
2. Taarifa ya viwango vya huduma ambavyo wateja wanatarajia kupatiwa kwa kuzingatia Maeneo Muhimu ya Matokeo na Malengo ya Mikakati yaliyokubaliwa katika Mpango wa Mkakati wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
3. Mipango ya kutatua matatizo endapo yatajitokeza na
4. Maelezo mafupi ya jinsi ya kutupata na kupata taarifa zaidi.

### Mapitio ya Mkataba

Tunatarajia kuupitia Mkataba huu kila mwaka. Tutafuatilia na kupitia utendaji wetu pamoja na mafanikio au matatizo ya Mkataba kwa kuwashirikisha wateja. Mkataba huu utawasaidia viongozi na wafanyakazi wetu kwa kuweka wazi huduma pamoja na viwango vya huduma hizo ambavyo tumejiwekea, lakini hasa ni kwa ajili ya wateja wetu. Ili ufanikiwe ni lazima uendelee kuboreshwa na kukidhi mahitaji ya wateja na Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

## MISINGI YA UTOAJI HUDUMA KWA UMMA NA WADAU WA HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA.

Chini ya Mkataba huu, Halmashauri ya Jiji la Mwanza imejiwekea misingi tisa ya utoaji huduma kwa umma na Wadau wake

Misingi hiyo ni:

1. Kuweka viwango vya huduma vilivyo wazi kwa wateja, kufuatilia utendaji na kuchapisha matokeo ya ufuatiliaji huu kwa kutumia wataalamu wa Halmashauri na wadau wengine kila inapowezekana.
2. Kuwa wazi na kutoa taarifa zote kwa wananchi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

   Tutakuwa wazi na kuwasiliana kwa ufasaha, na katika lugha inayoeleweka, kuwasaidia wananchi wanaotumia huduma za Halmashauri yetu, na tutawapatia wateja wetu taarifa zote kuhusu huduma zetu, gharama zake, na mafanikio yetu kila mwaka. Pamoja na kuwaalika katika vikao vyetu vya Full Council na kubandika taarifa muhimu katika mbao za matangazo za Kata na Halmashauri ya Jiji, kituo cha radio City fm na Tovuti. www.Mwanzacc.go.tz

1. Kushirikisha wengine

   Tutawashirikisha na kuwaomba ushauri watumiaji wa sasa na wa baadae wa huduma za Halmashauri ya JIji la Mwanza, pamoja na wafanyakazi wetu, na kutumia ushauri wao katika kuboresha huduma zetu.

2. Kukuza upatikanaji wa huduma

   Tutafanya jitihada kuhakikisha upatikanaji wa huduma zetu kwa kila anayezihitaji kwa urahisi zaidi. Tutajitahidi kukuza matumizi ya teknolojia kila inapowezekana, na kuwapa wateja wetu uwanja mkubwa zaidi wa kuchagua huduma kadri hali itakavyoruhusu.

3. Kuwatendea haki wote

   Tutawatendea watu wote haki, tutaheshimu utu wao na haki zao za binafsi, kuwasaidia kwa moyo, na kutoa kipaumbele kwa wale wenye mahitaji maalumu kama walemavu wa ngozi, wajawazito,waathirika wa Ukimwi na wateja wetu wengine wenye mahitaji maalumu.

4. Kutatua matatizo yanapojitokeza
   Tutajitahidi wakati wote kurekebisha mambo haraka na kwa uhakika, kujifunza kutokana na malalamiko, na kuwa na utaratibu wa kushughulikia malalamiko ulio wazi, rahisi kutumika na utakaosambazwa vema, ambao utawekwa wazi kwa ajili ya mapitio ya kila mara na wataalamu, wanasiasa na wadau wote.

5. Matumizi bora ya rasilimali
   Tutatumia rasilimali za fedha, watu na raslimali watu kwa namna itakayotoa matunda bora kwa walipa kodi, wafadhili na wateja na wadau wengine wote wa Halmashauri, ikiwa ni pamoja na serikali kuu.

6. Kuboresha huduma
   Tutajitahidi wakati wote kutafuta njia za kuboresha huduma zetu, kwa njia ya kushirikisha wadau.

7. Kushirikiana na watoa huduma wengine
   Tutafanya kazi na Halmashauri nyingine, Serikali Kuu na Wadau wengine, ili kuhakikisha kuwa huduma zetu ni rahisi kutumika na bora.

- Halmashauri itahakikisha kuna usawa wa Jinsia kwa watu wote katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

- Mifumo ya Utawala ya Wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Utazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utawala bora. Kifupi tutazingatia utawala wa kidemokrasia na utawala wa sheria.

**WATEJA WETU**

Tulipoanzisha Mpango wa Mkakati wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza tuliainisha wateja wetu pamoja na matarajio yao kama ifuatavyo:- Serikali za Mitaa/kata, Umma, Watumishi wa Umma, Wafadhili na watoa Msaada, Wanasiasa na Makundi mengine mbalimbali katika Jamii yetu ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Taifa kwa ujumla.

- Serikali za mitaa/kata
- Umma
- Watumishiwa umma
- Wafadhili

**Halmashauri ambayo ina haki ya kutarajia:-**

- Uwezo bora zaidi wa kubuni, kusimamia na kutathimini shughuli za maendeleo na utumishi bora unaozingatia utoaji wa huduma bora za kijamii na kiuchumi katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Ari kubwa zaidi na maadili bora kwa watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Kurekebishwa wakati kwa wakati kwa Ikama ya watumishi wa Halmashauri ili kuongeza uwezo wa kiutendaji na katika kutoa huduma bora za Kiuchumi, Kisiasa na Kiutamaduni, kulingana na mahitaji ya wananchi kwa ujumla.
- Matumizi bora ya nguvu kazi na usawa wa kijinsia katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

**Umma ambao una haki ya kutarajia:**

- Haki na uwazi kwa wananchi na wadau wake wote.
- Usawa wa Jinsia.
- Huduma bora kwa wadau wote katika Halmashauri.
- Staha kwa wananchi, katika Halmashauri na Taifa.
- Uaminifu.
- Kuheshimu sheria na
- Kupata habari mbalimbali kuhusu Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Matumizi bora ya taarifa za Halmashauri na Serikali kuu.

## VIWANGO VYETU

Kwa kuzingatia maadili haya muhimu, tunajitahidi wakati wote kuboresha kiwango cha huduma zetu kwenye maeneo ambayo tunaamini ni muhimu kwa wateja wetu, na ambayo huwa ni rahisi kupima matokeo yake na kupanga marekebisho.
Ubora wa mahusiano yetu na wadau wote.

- Ubora wa huduma tuzitoazo; na
- Kutoa huduma kwa wakati muafaka

**Watumishi wa Halmashauri wana haki ya kutarajia**

- Miundo sawa ya malipo inayohamasisha utendaji wao wa kazi
- Mfumo wa haki na ulio wazi wa utathimini utendaji kazi (OPRAS).
- Mfumo mzuri wa kuchunga / kudhibiti nidhamu kazini
- Kanuni zinazokwenda na wakati na taratibu bora za utawala na nguvu kazi
- Kuwepo na mchanganuo mzuri wa kazi ili kuwezesha mfumo mzuri wa utendaji.
- Kutoa taarifa sahihi za Ajira, uteuzi na upandishaji vyeo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Kuwepo kwa Uratibu wa mafunzo na maendeleo ya taaluma mbalimbali ili kupata ujuzi zaidi wa kutoa huduma bora.
- Viwepo viwango bora vya mazingira ya kufanyia kazi pamoja na vitendea kazi vilivyo bora na
- Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuweka kumbukumbu sahihi za Rasilimali watu na rasilimali nyingine za Halmashauri.
- Kuwalipa watumishi wote mishahara na mafao yao mengine ya kiutumishi kwa wakati.

**Wafadhili wana haki ya kutarajia**

- Utawala bora na uwazi.
- Huduma bora na za uhakika na
- Matumizi bora ya fedha za wafadhili

**Wanasiasa wana haki ya kutarajia:**

- Halmashauri ya Jiji la Mwanza isiyofungamana na siasa wala chama chochote.
- Matumizi mazuri katika shughuli zote za Halmashauri.
- Uwezo wa kufanikisha mipango ya maendeleo ya Halmashauri na serikali Kuu.
- Kuzingatia matakwa ya wananchi katika kupanga kusimamia na kutathimini maendeleo yao.

**HUDUMA ZETU**

Ili kukidhi matarajio haya ya wateja, Halmashauri imeainisha Maeneo Muhimu ya Matokeo Mpango Mkakati na Budget ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

**MALENGO YETU**

- Kusimamia vizuri kwa Bidii na Maarifa maendeleo ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Kuhakikisha kuwa watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza wana ari na moyo wa kujituma kazini katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Halmashauri kadri ya Budgeti na mpango mkakati wa Halmashauri.
- Kuwa na mfumo bora wa utoaji taarifa mbalimbali za Halmashauri.
- Kusimamia shughuli zote za maendeleo ya Kata na Mitaa ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

Ili kutekeleza malengo haya tutaongozwa na Dira na Mpango Mkakati wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

- Kuhakikisha wananchi na wadau mbalimbali wanashirikishwa katika maamuzi yanayofanywa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

**MAADILI MUHIMU YA HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**

- Utoaji wa huduma bora kwa wananchi wote.
- Utiifu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- Kujituma kazini kwa wataalamu na Madiwani
- Kutoa huduma bila upendeleo kwa wadau wote

**Mahusiano yetu na Majukumu yetu kwa Wateja wetu.**

Tunataka kuanzisha na kuendeleza mahusiano mazuri ya kikazi na wateja wetu kwa kupitia maelewano mazuri, nakutoa haki sawa kwa watu wote. Hapa chini tunaainisha tunachoona ni haki na majukumu ya wateja. Kwa upande wetu tunaahidi kutoa viwango vya juu kadiri inavyowezekana katika maeneo yafuatayo:-

- Kutoa huduma bora za maendeleo ya kijamii, kiuchumi, kiutamaduni katika Halmashauri yetu.
- Ushauri. Tutajitahidi wakati wote kutoa ushauri bora, mzuri, na uhakika na bila upendeleo kwa raia wote katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Tabia za Wafanyakazi. Tutawafundisha na kuwataka wafanyakazi wetu wawe marafiki, wasaidizi na wenye heshima kwa wateja; wakijitambulisha, kujieleza na kusikiliza kwa makini mahitaji na mawazo ya wateja na wadau wote wenye tija kwa maendeleo ya Halmashauri yetu.

**Ubora wa Viwango vya Huduma**

Tutajitahidi wakati wote kuongeza ubora wa huduma zetu katika maeneo yafuatayo:-

- Kuwajibika. Kusimamia Bajeti na mpango mkakati wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

- Matumizi ya lugha inayoeleweka. Tutahakikisha kuwa barua zote, fomu na machapisho pamoja na taarifa nyingine zinakuwa katika lugha inayoeleweka kadiri inavyowezekana na kwamba zinaweza kueleweka kwa walemavu na wadau wote.

- Uhakika: Tutafuatilia uhakika wa ushauri, taarifa au masuala yoyote yanayohusu raslimali watu, na raslimali fedha kwa manufaa ya Halmashauri na watu wake.

- Kutoa huduma kutokana na mahitaji, Tutahakikisha kuwa huduma zetu zinakidhi mahitaji ya wateja na mazingira waliyomo – hasa mahitaji maalum kwa walemavu na makundi mengine kama hayo.

**Viwango vya kutoa Huduma kwa Wakati Muafaka**
Hivi vinahusisha jinsi tunavyotoa huduma kwa haraka na kwa uhakika. Tutajitahidi kuboresha huduma zetu katika maeneo yafuatayo:-

- **Muda wa Kujibu Mawasiliano**
  Tutazishughulikia barua, barua pepe na simu zote haraka kadiri inavyowezekana na wakati wote kabla ya siku saba za kazi hazijapita tangu zitufikie.
- **Muda wa kutoa huduma muhimu**
  Tutasimamia mipango yote ya maendeleo ya Halmashauri kwa Mujibu wa Mpango mkakati wa Halmashauri na Budget ya Mwaka husika.

- Kushughulikia kero zote za Ardhi na kero nyingine za Maendeleo kwa wakati.

- Kuhakikisha uboreshaji wa utoaji huduma katika Idara na Vitengo vyote ya Halmashauri ya Jiji.

- Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma kwa umma ambazo sio lazima zitolewe na Serikali.

- Kuandaa na kukamilisha kwa program za mafunzo kwa watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza kila Mwaka.

- Kushughulikia nafasi za kwenda kusoma
  Kwa mujibu wa Mpango wa Mafunzo wa Halmashauri.
- Ajira mpya na kujaza nafasi zinazokuwa wazi kutokana na vifo, kujiuzulu na aina nyingine ya nafasi za kazi yatafanyika kwa kuzingatia Ikama na Budget ya Halmashauri.

**MALALAMIKO**

Utaratibu wetu wa kupokea malalamiko ya wateja na viwango wanavyoweza kutarajia malalamiko yao yashughulikiwe umeelezwa hapa chini. Tunaahidi kutoa taarifa za kupokelewa malalamiko yote ndani ya siku saba za kazi. Majibu, matokeo au taarifa ya maendeleo yatatolewa ndani ya siku 60.

**HAKI NA MAJUKUMU YA WATEJA**

Katika hati hii ya mkataba tumejaribu kueleza huduma tunazoweza kutoa kwa kuzingatia viwango ambavyo tunadhani wateja wana haki ya kuvitarajia kutoka kwetu, na katika hili tumewashirikisha. Pamoja na wateja kuwa na haki ya kupata huduma ya kiwango cha juu pia tunaamini wateja wana haki zifuatazo:-

- Kutotoa zawadi, upendeleo au vivutio kwa watumishi wa Halmashauri au kuomba vitu hivyo kutoka kwa watumishi wa Halmashauri.
- Kufanya vikao vyote vya kisheria toka ngazi ya mitaa, Kata na Halmashauri kwa wakati kwa Mujibu wa ratiba za vikao vya kisheria ya Halmashauri.
- Kutoa taarifa wanazoombwa na Serikali Kuu na Mamlaka nyingine kwa usahihi na kwa wakati muafaka na
- Kufuata taratibu za kisheria katika kufanya malipo ya mafao mbalimbali ya watumishi, malipo ya wazabuni na matumizi mengineyo kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Serikali.

Tunakaribisha Malalamiko:

Tunakaribisha wakosoaji wenye nia ya kujenga au kutueleza maendeleo ya huduma zetu; kama vile ambavyo pia tunakaribisha wale wenye kutusifia na kutoa mapendekezo ya namna tunavyoweza kuboresha huduma zetu. Zaidi ya hayo tunaahidi kuwa malalamiko na mapendekezo haya yatachukuliwa kwa umuhimu na kushughulikiwa haraka iwezekanavyo na afisa anayehusika.

**Jinsi ya kutuma Malalamiko**

Malalamiko yanaweza kutumwa kwa posta, simu, faksi au barua pepe, au kwa mhusika mwenyewe kuyaleta kwa kupitia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji
S.L.P. 1333
MWANZA

Simu: 255-28-2501375

Fax: 255-028-2500785

*Barua Pepe:* E-mail. info@mwanzacc.go.tz

**Namana ya Kutoa Mlishonyuma Kuhusu Maendeleo ya Mkataba**

Halmashauri ya Jiji la Mwanza inakaribisha taarifa kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Taarifa hiyo iwe ya kweli na iwe inahusu huduma zetu na viwango vinavyotarajiwa kuvifikia. Lakini pia iwe inahusu jinsi wateja wanavyoweza kuchangia katika kuboresha viwango hivi. Mapendekezo yatumwe kwenye anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Jiji
S.L.P. 1333
MWANZA

Simu: 255-28-2501375

Fax: 255-028-2500785

*Barua Pepe:* E-mail. info@mwanzacc.go.tz

**Kumbukumbu za Malalamiko**

Tunaweka kumbukumbu za malalamiko, changamoto pamoja na mapendekezo yote. Hizi zitatumika kwa ajili ya ufuatiliaji wetu wa ndani, na kutusaidia katika kuboresha huduma kwa wateja. Pamoja na kuwa tunategemea na kuwataka walalamikaji wote wajitambulishe tunawahakikishia kuwa taarifa zote, ikiwa ni pamoja na majina vitakuwa ni siri.

**Kukata Rufaa**

Ingawa tuna mfumo wa utatuzi wa malalamiko ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza, hii haimzuii mteja kutumia vyombo vingine nje ya mfumo huu ili kutafuta jawabu kwa yatakayojitokeza kama vile Tume ya Haki za Binadamu, ambayo anwani yake ni:-

Tume ya Haki za Binadamu,

S.L.P. 2643

Dar Es Salaam

Tanzania

Simu: (+255)0222110607 au 2110141

**MAPITIO YA MKATABA**

**Lengo la Kupitia**

- Mkataba huu utabadilika wakati kwa wakati ili kwenda na wakati na kutilia maanani mabadiliko ya Kiuchumi, Kisiasa na Kiutamaduni.
- Unaendelea kutoa mtazamo wetu katika suala zima la huduma kwa wateja, au msukumo mwingine wowote mpya katika eneo hili hasa kuhusu maendeleo ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Malengo na viwango vya huduma bado vinakwenda sambamba na mahitaji na matarajio ya mteja na washikadau muhimu. Tunakaribisha mapendekezo kutoka kwa wadau wote wa Halmashauri.
- Kama bado Mkataba huu unakidhi misingi ya huduma kwa wateja.
- Yaliyomo kwenye mkataba bado ni sahihi.
- Mfumo na utaratibu uliotumika kuandika mkataba unakidhi mahitaji ya mteja.
- Tuna mfumo mzuri wa kufuatilia maendeleo ya mkataba toka kwa wateja, viwango vya huduma na malalamiko ya wateja na
- Iwapo kuna haja ya kufanya mabadiliko ya mbinu zetu za kutatua matatizo ya wateja.

## UTOAJI WA TAARIFA

I. Mbao za matangazo zilizopo kwenye jengo la Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
II. Mbao za matangazo zilizopo katika Ofisi za Kata ya Mitaa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
III. Kituo cha Radio cha Halmashauri ya Jiji la Mwanza (CITYfm, 90.Ifm)
IV. Tovuti Ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza ( Www.Mwanzacc.go.tz)
V. Vituo mbalimbali vya Televisheni na Magazeti.

### Ushauri katika Mapitio

Ili tuwe wazi na tuwajibike, tutaomba ushauri kwa wateja na washika dau katika zoezi zima la mapitio; na pia vyombo vingine kama vile Tume ya Haki za Binadamu, pamoja na kufanya tafiti kuhusu huduma tunazotoa.

- Tutachapisha maendeleo kwa kulinganisha na malengo ya mkataba wetu katika bajeti ya kila Mwaka ya Halmashauri.
- Tutatoa taarifa za maendeleo ya mkataba kwa wateja na washika dau muhimu (pamoja na wafanyakazi wetu). Hii itasaidia kukuza uwazi na uwajibikaji ili kuendeleza mahusiano ya wateja, washikadau na wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza.
- Tutachapisha taarifa fupi kuhusu malalamiko, na jinsi yanavyoshughulikiwa katika taarifa za kila Mwaka.
- Tutatoa taarifa fupi kila Mwaka TAMISEMI/Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu utekelezaji wa mkataba wetu wa huduma kwa mteja.

Kiomoni Kiburwa Kibamba

**MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA**

MKURUGENZI WA JIJI LA MWANZA
MWANZA

James Bwire
**MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA JIJI
MWANZA**

HON MAYOR
MWANZA CITY COUNCIL
MWANZA

05 Januari, 2018